# Fomu ya Uthibitisho wa Mzazi/Mwanafunzi

**Je, MAP ni nini?**
MAP ni mtihani wa kompyuta, ambayo inamaanisha kila mwanafunzi anapata seti ya kipekee ya maswali ya mtihani kulingana na majibu ya maswali ya awali. Mwanafunzi anapoendelea kujibu kwa usahihi, maswali yanaendelea kuwa magumu. Ikiwa mwanafunzi hatajibu kwa usahihi, maswali yanaendelea kuwa rahisi. Mwisho wa mtihani, wanafunzi wengi watajibu karibu nusu ya maswali kwa usahihi.

**Je, MAP hutathmini nini?**
Matoleo ya MAP hutolewa kama alama ya nambari ya RIT. Alama hii hutumiwa kuangalia kiwango cha mafanikio cha mwanafunzi nyakati tofauti za mwaka wa shule na kubainisha ukuaji. Fikiria kuhusu hii kama kuweka alama ya urefu kwenye chati ya ukuaji. Unaweza kuelezea urefu wa mtoto wako katika nyakati tofauti na kiwango alichokua kati ya wakati mmoja na mwingine.

**Alama ya RIT ni nini?**
Mizani ya RIT (Kizio cha Rasch) ni mizani thabiti yenye ulinganisho sawa, kama futi na inchi. Ulinganisho sawa humaanisha kwamba mabadiliko ya pointi 10 za RIT huashiria kitu kimoja haijalishi kama mwanafunzi ako juu, chini au katikati kwenye mizani, na alama ya RIT ina maana moja haijalishi kiwango cha gredi au umri wa mwanafunzi. Alama baada ya muda zinaweza kulinganishwa ili kuelezea jinsi ukuaji wa kielimu wa mwanafunzi unavyofanywa, sawa na kupima urefu kwa kutumia rula.

**Walimu hutumia aje alama za MAP?**
Walimu wanaweza kuona maendeleo ya kila mwanafunzi na darasa lao kwa ujumla. Wanafunzi wenye alama sawa kwa kawaida huwa tayari kusoma katika stadi na mada sawa. Pia MAP hutoa data inayohusu ukuaji wa kawaida wa wanafunzi ambao wako katika gredi moja, na wanasomea mada moja, na wana kiwango sawa cha kuanzia cha ufanisi. Data hii hutumiwa mara kwa mara kuwasaidia wanafunzi kuweka malengo na kuelewa wanachohitajika kujifunza ili kutimiza malengo yao.

**Mtihani wa MAP huchukua muda gani na mtoto wangu atalazimika kufanya mitihani hii mara ngapi?**
Mitihani huwa haina muda, na wanafunzi wanaweza kuchukua muda mwingi kama wanavyohitaji ili kuikamilisha. Wanafunzi wengi huchukua chini ya saa moja kukamilisha mtihani wa MAP. Mitihani hii hupeanwa katika Shule ya chekechea na gredi ya 1 na kwa kawaida huchukua muda mfupi.

**Je, ni maelezo gani nitakayoyapokea kutoka kwa shule ya mtoto wangu?**
Utapewa Ripoti ya Maendeleo ya Mwanafunzi ya mtoto wako. Ripoti hii ina maelezo na alama kutoka kwa mitihani ya hivi karibuni na ya zamani ya mtoto wako ya mitihani ya MAP.

**Ninawezaje kumsaidia mtoto wangu kujiandaa kwa mitihani ya MAP?**
Mwalimu wa mtoto wako atasaidia na maagizo yoyote ya kabla ya mtighani ili kuelezea mtihani kwa wanafunzi. Kama vile siku nyingine yoyote ya shule hakikisha mtoto wako amepumzika vya kutosha na amelishwa vyakula vizuri. Mhimize kufanya vizuri kama awezavyo. Huu si mtihani rasmi lakini zana inayotumiwa kutathmini ni nini mwanafunzi anachojua na anachopaswa bado kujifunza.

**Usalama wa Mtihani kwa Mtihani wa MAP wa Wanafunzi**
Sehemu hii kuhusu usalama inajumuisha maelezo ambayo yanatumika kwa wazazi na wanafunzi. Maelezo haya yanalenga kukusaidia kuelewa taratibu ambazo waratibu wa mtihani hutumia ili kuwafahamisha kuhusu majukumu yao, na majukumu nyumbani wakati wa utekelezaji wa tathmini.

Ifuatayo ni orodha ya vitu vinavyopaswa kuzingatiwa kabla ya mtihani. Orodha hii inapaswa kuchukuliwa kuwa ni kamili.

**Mambo ambayo ni Lazima Uyafanye:**
Maandalizi Nyumbani:

- Tekeleza kaguzi zote muhimu za teknolojia kuwa tayari.
    - Ufikiaji wa Intaneti
    - Upatikanaji wa kompyuta
    - Betri ya kompyuta iliyochajiwa kabisa
- Hakikisha mwanafunzi ana mahali patulivu pa kufanyia mtihani, mbali na usumbufu wote.
- Hakikisha kwamba mwanafunzi anaweza kuonekana vizuri na mtahini wa mtihani kupitia kamera ya kompyuta, KILA WAKATI.
- Fuata sera na maagizo ya kikokotoo na vifaa vya elektroniki.
- Thibitisha kwamba mwanafunzi ana nyenzo zote za mtihani, kama ilivyoelezewa na mtahini wa mtihani.
    - Karatasi ya Mazoezi
    - Penseli
    - Vifaa vya masikio (Kwa shule ya chekechekea, gredi ya 1, gredi ya 2, na wanafunzi wanahitaji vifaa vya masikio kulingana na mpango wao wa EP, 504-IAP, na/au EL-TPC). Tafadhali wasiliana na shule ya eneo lako ikiwa vifaa vya masikio vinahitajika.

**Mambo ambayo Hupaswi Kufanya:**
Maudhui ya Mtihani:

- Kuwapa wanafunzi jibu, au vidokezo vyovyote vya majibu, kwa swali lolote la mtihani.
- Kuandika manukuu kuhusu maudhui ya mtihani wakati wa utekelezaji mtihani.
- Kutumia maelezo yoyote kuhusu maswali halisi ya mtihani, haijalishi yalipatikana aje, ili kuwasaidia wanafunzi kujiandaa kwa mtihani. Maelezo kama hayo hayawezi kushirikiwa na mtu yeyote kwa malengo yoyote, ikiwemo kupitia mitandao na mawasiliano ya kijamii.

Utekelezaji wa Mtihani:

- Kuingia/kutatiza mazingira ya mtihani wakati wa utekelezaji wa mtihani isipokuwa iwe ni kwa sababu ya hali ya dharura au mahitaji mengine muhimu ambayo yanaathiriwa na muda.
- Kumwondoa/kusababisha mwanafunzi kuondolewa mbali na macho ya mtahini wa mitihani.

Nimesoma yaliyo hapa juu na ninaelewa majukumu yangu katika kuhakikisha mazingira salama, mazuri na yasiokuwa na usumbufu wowote kwa wanafunzi wafuatao:

Mwanafunzi: ______________________ Gredi: ___________ Mwalimu kwenye Rekodi. _______________

Jina la Mzazi: ___________________________ Shule: _____________________________ Tarehe:__________